

# **HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE**

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Anuani ya Simu:

Simu: +255 659 566703

Fax:

Email: [ded@sikongedc.go.tz](mailto:ded@sikongedc.go.tz).



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),

S.L.P. 70,

**SIKONGE**

27/05/2019

## **TANGAZO LA KAZI.**

MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE ANAWATANGAZIA NAFASI ZA KAZI ZIFUATAZO WATANZANIA WENYE SIFA ZILIZOTAJWA HAPA CHINI; KWA KILA KAZI. WAOMBEJI WAWASILISHE BARUA YA MAOMBI KWA KUTUMIA ANUANI ILIYOPO CHINI IKIAMBATANISHWA NA SIFA BINAFSI (CV) PAMOJA NA NAKALA ZA VYETI VYA ELIMU NA TAALUMA ALIYONAYO.

**MWISHO WA KUWASILISHA MAOMBI NIA TAREHE  
14/06/2019 SAA 9.30 MCHANA.**

### **1. AFISA NYUKI DARAJA II - NAFASI 1**

#### **SIFA ZA MWOMBAJI:**

- Awe na Shahada katika fani ya ufugaji nyuki
- Awe na Sayansi ya Elimu ya mimea,
- Awe na Elimu ya Wadudu
- Awe na Elimu ya Wanyama kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali

#### **KAZI NA MAJUKUMU**

1. Kusimamia uanzishaji wa hifadhi za nyuki na manzuki
2. Kutangaza sera, sheria za ufugaji nyuki
3. Kufundisha masomo ya fani ya ufugaji nyuki
4. Kukusanya takwimu za rasilimati na ufugaji nyuki
5. Kupanga na kupima ubora wa mazao ya nyuki

#### **AINA YA AJIRA**

Ajira ya Mkataba (Contract)

#### **MSHAHARA:**

Tsh. 500,000/= kwa mwezi kulingana na viwango vilivyoidhinishwa na Baraza la Madiwani

## 2. MHANDISI (UJENZI) DARAJA II - NAFASI 1

### SIFA ZA MWOMBAJI:

- Awe na Shahada Stashahada ya Juu ya Uhandisi kutoka vyuo vikuu vinavyotambuliwa na Serikali katika mojawapo ya fani za Uhandisi

### KAZI NA MAJUKUMU

1. Kufanya ukaguzi wa Barabara, madaraja na majengo mbalimbali.
2. Kufanya kazi chini ya uangalizi wa Mhandisi aliyesajiriwa (Professional Engineer) na bodi ya usajili ya Wahandisi ili kupata uzoefu unaotakiwa.
3. Kuchunguza vyanzo vya ajali barabarani
4. Kufuatilia utekelezaji wa sheria na kanuni za ujenzi wa Barabara na Majengo.
5. Kutayarisha bajeti ya mwaka ya ujenzi na matengenezo ya Barabara, Madaraja na Majengo.
6. Kusimamia na kuratibu kazi za Barabara, Madaraja na Majengo zinazotolewa na Makandarasi.

### AINA YA AJIRA

Ajira ya Mkataba (Contract)

### MSHAHARA:

Tsh.500,000/=kwa mwezi kulingana na viwango vilivyoidhinishwa na Baraza la Madiwani

**Barua za Maombi zitumwe kwa:-**

**Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge,  
S.L.P 70,  
SIKONGE.**

**Tangazo limetolewa Na:-**



Eng. Paschal Ngunda  
Kaimu Mkurugenzi Mtendaji  
**SIKONGE.**

MKURUGENZI MTENDAJI WILAY/

SIKONGE.